**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**BUNGE LA TANZANIA**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

## MKUTANO WA ISHIRINI

## KIKAO CHA ISHIRINI

**04 JUNI, 2015**

# ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO

---

## MKUTANO WA ISHIRINI

### KIKAO CHA ISHIRINI– TAREHE 04 JUNI, 2015

## I. MASWALI YA KAWAIDA:

### OFISI YA WAZIRI MKUU:

**135. MHESHIMIWA MARIAM NASSORO KISANGI (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Liko tatizo kubwa la nyumba za Walimu wa Shule za Msingi na Sekondari nchini hasa kwa wale walioko mijini:-

(a) Je, kwa nini Serikali kupitia mpango wake wa kuboresha makazi kupitia **NHC** isiwape Walimu kipaumbele;

(b) Je, kwa nini Serikali isiwaunganishe Walimu moja kwa moja na benki zinazotoa mikopo ya nyumba, wawaelimishe na ikiwezekana wawajengee Walimu nyumba za gharama nafuu kwa masharti nafuu na malipo ya muda mrefu.

**136. MHESHIMIWA MARIAM REUBEN KASEMBE (MASASI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:- Serikali ilitoa agizo kwamba kila Jumamosi ya mwisho wa mwezi ni siku ya usafi wa mazingira kwa nchi nzima:-

Je, ni Wilaya ngapi zinatekeleza agizo hilo na hali ya usafi ikoje kwa sasa.

**137. MHESHIMIWA MESHACK JEREMIAH OPULUKWA (MEATU):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri Mkuu:-

Mbunge kwa nafasi yake ni Diwani katika Halmashauri yake; Je, ni vikao vipi vya Halmashauri ambavyo Mbunge haruhusiwi kuhudhuria na ni kwa nini.

## WIZARA YA KILIMO, CHAKULA NA USHIRIKA:

**138. MHESHIMIWA ASAA OTHMAN HAMAD (B.L.W):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Mabadiliko ya tabianchi yamekuwa matatizo makubwa hasa kwa nchi zinazoendelea ikiwemo Tanzania; na nchi

yetu licha ya kujaaliwa rasilimali kama vile Misitu, Mito na Maziwa makubwa bado kuna maeneo yanayorejesha nyuma shughuli za kilimo kwa Wananchi wa maeneo hayo:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa muda mfupi, muda wa kati na muda mrefu wa kuzitumia ardhi hizo kwa kilimo;

(b) Je, ile dhana ya kuvuna maji ya mvua imeishia wapi.

**139. MHESHIMIWA EZEKIEL MAGOLYO MAIGE (MSALALA):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Kilimo, Chakula na Ushirika:- Bei ya zao la Pamba imekuwa ikishuka mara kwa mara na kusababisha hasara kwa wakulima:-

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka utangamano wa uzalishaji na bei (price and production stability) kwa zao hilo;

(b) Je, Serikali inaweza kutoa fidia ya hasara inayotokana na tofauti ya gharama ya uzalishaji na mauzo inayofikia kiasi cha shilingi 52,000/=;

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhamasisha uzalishaji wa mazao mengine ya biashara kama Alizeti ambayo yanastahimili ukame wa Mkoa huo.

## WIZARA YA UJENZI:

**140. MHESHIMIWA DKT. CHRISTINE GABRIEL ISHENGOMA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-
Serikali imefanya kazi nzuri sana katika ujenzi wa barabara hapa nchini:-

(a) Je, ni lini ujenzi wa barabara ya Turiani hadi Mikumi kwa kiwango cha lami utaisha;

(b) Je, ni sababu gani zilizopelekea kusimama kwa ujenzi wa barabara hiyo.

**141. MHESHIMIWA JOSEPH OSMUND MBILINYI (MBEYA MJINI):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Ujenzi:-
Kwa miaka mingi sasa katika Jiji la Mbeya kumekuwa na ongezeko kubwa la watu na magari, jambo linalosababisha ajali hasa katika makutano ya Barabara Kuu iendayo Zambia katika eneo la Mafiati:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kuweka taa za kuongozea magari *(traffic lights)* katika eneo hilo ili kupunguza ajali na msongamano wa magari katika eneo hilo.

## WIZARA YA AFYA NA USTAWI WA JAMII:

**142. MHESHIMIWA BETTY ELIEZER MACHANGU (VITI MAALUM)**:

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Afya na Ustawi wa Jamii:- Hospitali ya KCMC ni Hospitali kubwa inayotoa huduma kwa watanzania na kwa wagonjwa kutoka nchi jirani lakini haina Kitengo cha Magonjwa ya Akili, isipokuwa kinategemewa kile kilichopo katika Hospitali ya Rufaa ya Mkoa – Mawenzi ambacho ni kidogo sana na hakina wataalamu wa Magonjwa ya Akili:-

(a) Kwa kuwa Kitengo hicho ni cha Muhimu sana hasa kwa Kanda ya Kaskazini; Je Serikali itakuwa tayari kuunga mkono kifedha juhudi za Bodi ya Wadhamini ya KCMC kuanzisha Kitengo hicho;

(b) Je, Serikali iko tayari na ni lini itakiboresha kitengo cha Magonjwa ya Akili kilichopo katika Hospitali ya Mawenzi kwa kukipatia Wataalamu waliobobea wa Magonjwa hayo.

## WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO:

### 143. MHESHIMIWA MARGARETH AGNES MKANGA (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo:-

Wanamichezo wenye ulemavu hasa michezo ya *Paraolimpic* wamekuwa wakifanya vizuri kwenye mashindano ya Kimataifa licha ya changamoto nyingi zinazokabili timu zao wakati wa maandalizi:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuwawezesha wananchi hao kuondokana na changamoto hizo.

## WIZARA YA UCHUKUZI:

### 144. MHESHIMIWA AMINA NASSORO MAKILAGI (VITI MAALUM):

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Uchukuzi:**-** Ilani ya CCM ya Mwaka (2010 - 2015) Ibara ya 67(d) inatamka juu ya kujenga Miundombinu ya Reli na Bandari:-

a) Je, ni lini Serikali itajenga Miundombinu ya Reli na Bandari kwa kukamilisha mtandao wa Meli na kuunganisha Bandari ya Tanga na Reli ya Arusha – Musoma;

b) Je, ni lini Serikali itajenga Bandari ya Mwambani Tanga pamoja na Reli mpya kati ya Arusha – Musoma.

**WIZARA YA MAMBO YA NDANI YA NCHI:**

**145. MHESHIMIWA FELIX FRANCIS MKOSAMALI (MUHAMBWE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Kumekuwepo na matukio mengi ya ujambazi katika Wilaya ya Kibondo ambayo iko mpakani mwa nchi:-

(a) Je, tangu mwaka 2010 hadi sasa, ni matukio mangapi yanayohusu ujambazi, utekaji magari na kuvunjwa kwa maduka ya Wananchi ambayo yametokea;

(b) Je, hali hiyo inasababishwa na nini na Serikali imechukua hatua gani;

(c) Ikiwa usalama wa raia ni jukumu la msingi la Serikali; Je, ni lini Serikali itahakikisha Wananchi wa Kibondo wanapata usalama kama raia.

**146. MHESHIMIWA CLARA DIANA MWATUKA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi:- Tanzania inajulikana duniani kote kwa kuwa kisiwa cha AMANI na UTULIVU; lakini hivi karibuni kumeshamiri vitendo vha ukatili na mauaji kote nchini hali inayohatarisha kutoweka kwa sifa hiyo ya amani na utulivu:-

Je, Serikali inachukua hatua gani juu ya vitendo hivyo ili kuhakikisha sifa hii ya amani na utulivu haipotei nchini.

## WIZARA YA FEDHA:

**147. MHESHIMIWA MARTHA JACHI UMBULLA (VITI MAALUM):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:- Serikali ilihamasisha uanzishwaji wa SACCOS na taasisi binafsi, NGOs za fedha ili kutoa mikopo kwa wajasiriamali wadogowadogo na nyingi zimefanikiwa sana ikiwemo ile ya WEDAC; lakini changamoto inayokabili WEDAC na SACCOS Mkoani Manyara hususan Kata za Dongobesh, Hydom, Maretadu, Manghang', Tumati, Endamitay, Bashay na Yaedachini ni ukosefu wa Benki, kwani benki iliyopo ipo kwenye Makao Makuu ya Wilaya ya Mbulu ambako ni mbali sana kutoka kwenye Kata hizo:-

Je, Serikali ina mikakati gani ya kuanzisha tawi la benki katika Kata ya Dongobesh ambako kuna vigezo vyote vya kuwezesha kuanzishwa kwa benki kuhudumia Kata zilizotajwa na maeneo jirani nazo.

**148. MHESHIMIWA MASOUD ABDALLAH SALIM (MTAMBILE):**

Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Fedha:- Ni mara kadhaa Serikali imekuwa ikiahidi kwamba ina mkakati wa kuwatunza na kuwaenzi wastaafu wake ili kukabiliana na kupanda kwa gharama za maisha:-

Je, Serikali imejiandaa vipi kutelekeza ahadi yake hiyo.

## II. HOJA ZA SERIKALI:

**WAZIRI WA AFYA NA USTAWI WA JAMII:**

Kwamba, Bunge sasa likubali kujadili na kupitisha Makadirio ya Matumizi ya Wizara ya Afya na Ustawi wa Jamii kwa Mwaka wa Fedha 2015/2016.

***(Majadiliano yanaendelea)***

**DODOMA** **DKT. T. D. KASHILILAH**
**04 JUNI, 2015** **KATIBU WA BUNGE**